**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# MWONGOZO WA UDHIBITI WA MAAMBUKIZI YA COVID-19 KATIKA SHULE, VYUO NA TAASISI ZA ELIMU NCHINI

**Toleo la Pili la 25 Juni 2020**

## 1. UTANGULIZI

Kufuatia mlipuko wa ugonjwa wa Homa kali ya Mapafu inayosababishwa na Virusi vya Corona (COVID-19) ulioripotiwa kwa mara ya kwanza nchini tarehe 16 Machi, 2020, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kwa ajili ya kudhibiti kuenea kwa ugonjwa huu. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kufunga shule zote za Awali, Msingi, Sekondari, Vyuo na taasisi za Elimu nchini. Aidha, kutokana na takwimu za mwenendo wa ugonjwa huu nchini kwa sasa kuonesha kupungua kwa maambukizi ya virusi vya Corona, mnamo tarehe 20 Mei 2020, Mhe. Dkt John Pombe Magufuli Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alitangaza kurejesha ratiba za masomo kwa shule za Sekondari (Kidato cha 6), Vyuo na Taasisi za Elimu kuanzia tarehe 01 Juni 2020. Aidha, katika Hotuba yake ya kulivunja Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 16 Juni 2020, Mhe Rais alitangaza kufungua shule zote kwa madarasa yaliyosalia ambayo ni Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana (Day Care Centre), Vituo vya watoto wachanga (crèche), Shule za Mafundisho ya Kidini, Shule za Awali, Msingi na Sekondari kuanzia tarehe 29 Juni 2020. Kufuatia hatua hiyo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeona ipo haja ya kupitia toleo la kwanza la Mwongozo wa Udhibiti wa Maambukizi ya COVID-19 katika Shule, Vyuo na Taasisi za Elimu na kuandaa toleo la pili.

Toleo la Pili la Mwongozo wa Udhibiti wa Maambukizi ya COVID-19 katika Shule, Vyuo na Taasisi za Elimu nchini linaongeza msisitizo na kuweka utaratibu wa nyongeza kwa Vituo vya kulelea watoto wadogo mchana (Day Care Centre), Vituo vya watoto wachanga (crèche), Shule za Awali na

Msingi, Shule za mafundisho za kidini ili kuendelea kukinga na kudhibiti maambukizi ya virusi vya Corona nchini.

## 2. MAMBO YA KUZINGATIA

Katika kufanikisha uwepo wa mazingira wezeshi na salama, Mwongozo huu umebainisha maeneo makuu manne ambayo yamebainisha mambo ya kuzingatia. Maeneo hayo ni Maandalizi ya mazingira ya shule kabla ya kufunguliwa, Uchunguzi wa Afya, Usafiri wa kwenda na kurudi shule na Mazingira ya kujifunzia kama inavyofafanuliwa kama ifuatavyo: -

### 2.1 Maandalizi ya Mazingira ya shule kabla ya kufunguliwa

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara zote zinazosimamia shule na Vituo vya Elimu wanatakiwa kuhakikisha uwepo wa mazingira salama kabla wanafunzi hawajarejea ili kudhibiti maambukizi mapya ya ugonjwa wa COVID-19. Katika kuandaa mazingira, mambo yafuatayo yanatakiwa kuzingatiwa;

- Kutakasa mazingira yote ya shule. vyuo na Vituo (Decontamination) kwa kuzingatia miongozo ya utakasaji iliyotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Hii inahusisha shule ambazo zilitumika kutunza washukiwa au wagonjwa wa Corona, utakasaji huu ufanyike angalau saa 72 kabla ya wanafunzi kuingia.
- Siku ya kwanza ya kufunguliwa Shule, Vyuo na Vituo vya Elimu ni muhimu itumike kutoa elimu kwa wanafunzi, wafanyakazi, wasaidizi wa wanafunzi wa watu wenye ulemavu kuhusu ugonjwa wa COVID-19 pamoja na dalili zake na hatua za kuchukua ili kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu
- Kuhakikisha uwepo wa vifaa vya kunawia mikono (sabuni na maji tiririka) kwa ajili ya usafi wa mikono katika kila eneo au maeneo ya madarasa, ofisi, kila geti/lango kuu, kila bweni, maktaba, bwalo la chakula, vyoo na maeneo mengine muhimu. **Wizara inasisitiza matumizi ya sabuni na maji tiririka ndio iwe njia kuu ya usafi wa mikono. Vilevile vifaa vya kunawa mikono vizingatie mahitaji ya wanafunzi wenye ulemavu na Watoto wadogo.** Aidha, vitakasa mikono (hand sanitizer) vinaweza kutumika kama mbadala wa maji tiririka na sabuni.
- Uongozi wa Shule na Vituo uhakikishe vitakasa mikono (*hand sanitizer*) vinavyotumika vina ubora unaotakiwa (**iliyotengenezwa kwa *ethanol* yenye asilimia zaidi ya 70**). Matumizi ya vitakasa mikono ni **suala la hiari** kwa mwanafunzi kwa sababu Wizara tunasisitiza zaidi matumizi ya **maji tiririka na sabuni**.

- Spirit *(Methanol)* isitumike kama kitakasa mikono katika maeneo yote ya shule/Chuo. Wanafunzi wasiagizwe kwenda na *spirit* shuleni. Uongozi wa Shule/Chuo uhakikishe wanafunzi hawaingii na *spirit* katika maeneo yao.
- Shule na Vyuo vyenye vituo vya kutolea huduma za afya, watumishi wote wanaohusika wapewe elimu juu ya kuwahudumiwa wanafunzi, walimu na wafanyakazi wote watakaoshukiwa kuwa na *COVID-19* ikiwemo kuwapatia msaada wa kisaikolojia na kuondoa unyanyapaa. Aidha, Shule na Vituo hivi vinapaswa kuwa na dawa na vifaa kwa ajili ya dharura.
- Uongozi wa Shule, Vyuo na Vituo vinavyotoa huduma za Bweni wanafunzi/watoto wadogo na wachanga uhakikishe kadri inavyowezekana kunakuwepo na nafasi ya mita moja kati ya kitanda kimoja hadi kingine na kudhibiti uchangiaji vifaa kwa wanafunzi kama vile taulo, mashuka, vyombo vya kuogea na vifaa vya usafi wa mwili.
- Uongozi wa Shule, Vyuo na Vituo uhamasishe wanafunzi, walimu na wafanyakazi wao wakiwemo wasaidizi wa wanafunzi wenye ulemavu wanavaa barakoa za vitambaa (*Cloth masks*) wakati wanaporudi shuleni na wanapohudumia watoto. Aidha, wazazi/walezi wahimizwe kuwapatia watoto wao barakoa za vitambaa kabla ya kwenda shuleni.
- Uongozi wa Shule, Vyuo na Vituo vya Elimu uweke utaratibu mzuri wa upatikanaji wa barakoa za vitambaa (*Cloth Masks)* zinazotengenezwa nchini na ambazo vinaweza kufuliwa na kupigwa pasi kila siku katika maeneo yao kwa gharama nafuu. Barakoa za vitambaa vya pamba zenye safu kuanzia mbili (two layers) ndizo zinazoshauriwa kuvaliwa kwa kuwa ni bora na salama kiafya na zinaweza kunyooshwa ipasavyo. Wazazi wanaweza kuwapa au kuwanunulia watoto wao.

- Uongozi wa Shule, Vyuo na Vituo vya Elimu unapaswa kuhakikisha uwepo wa vifaa vya kuhifadhia taka zitokanazo na barakoa zilizotumika na kuziteketeza kama taka nyingine hatarishi ili kuzuia maambukizi ya virusi vya Corona.

### 2.2 Uchunguzi wa Afya

- Wanafunzi watakaohisiwa kuwa na dalili za COVID-19 wazazi au walezi watoe taarifa ili wafanyiwe vipimo kabla ya kurudi shuleni ili watakaobainika kuwa na maambukizi wabaki nyumbani hadi hapo hali zao za afya zitakapoimarika
- Uongozi wa shule/Chuo uhakikishe wanafunzi ambao watabainika kuwa na dalili za ugonjwa wa Corona wakiwa Shuleni wanatolewa taarifa kwenye kituo cha huduma za afya kilicho karibu nao kwa ajili

ya uchunguzi na matibabu zaidi na kuwajulisha wazazi au walezi wa mtoto kwa mashauriano zaidi.

- Uongozi wa Shule/Chuo husika umwangalie mwanafunzi atakayebainika kuambukizwa kwa ukaribu kipindi chote cha shule na anapokuwa kituo cha matibabu au kadri ya ushauri wa wazazi au walezi wa mwanafunzi.

### 2.3 Usafiri wa kwenda na kurudi shuleni

- Wamiliki wa magari ya Shule (School bus) waweke vitakasa mikono kwenye magari yao kwa ajili ya wanafunzi wakati wa kupanda kuelekea shuleni.
- Wamiliki wa magari ya Shule (School bus) wahakikishe kuwa abiria na wahudumu wote wanavaa barakoa za vitambaa na kutumia vitakasa mikono kabla ya wanafunzi kupanda gari husika.
- Kwa wanafunzi watakaopanda mabasi ya abiria maarufu kama daladala kwenda mashuleni na kurudi majumbani utaratibu wa sasa wa usafiri utatumika ambapo kila mmiliki wa basi la abiria anawajibika kutii maelekezo ya usalama kwa abiria kama yanavyotolewa na Mamlaka husika.

### 2.4 Mazingira ya kujifunzia

- Uongozi wa Shule, Vyuo na Vituo unapaswa kuhimiza na kuwasimamia wanafunzi, walimu na watumishi wao kuzingatia Kanuni za Usafi binafsi ikiwemo kunawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na sabuni kabla ya kuingia getini/lango kuu, darasani, bwenini, maktaba, bwalo la chakula, ofisini na maeneo mengine muhimu.
- **Kwa watoto wadogo kwenye shule za awali, vituo vya kulelea watoto wadogo na wachanga wanatakiwa kusaidiwa kwenye unawaji wa mikono kama inavyotakiwa.** Wizara inasisitiza matumizi ya sabuni na maji tiririka ndiyo iwe njia kuu ya usafi wa mikono. Aidha, Vitakasa Mikono (Hand sanitizer) vinaweza kutumika kama mbadala wa maji tiririka na sabuni. Inaelekezwa walimu wa madarasa wakisaidiana na viongozi wa wanafunzi/viranja wahakikishe haya yanasimamiwa ipasavyo.
- Uongozi wa Shule, Vyuo na Vituo vya Elimu unapaswa kuhakikisha, kadri inavyowezekana, watumishi wote na wanafunzi wanakaa/kusimama kwa umbali wa mita moja au zaidi kati ya mtu mmoja na mwingine wawapo sehemu yoyote wakati wa mafunzo na wakati wa mazoezi.
- Uongozi wa Shule, Chuo na Vituo vya Elimu uhakikishe wanafunzi, walimu na wafanyakazi wao wanavaa barakoa za vitambaa (*Cloth*

*masks)* wakati wawapo shuleni hususani wanapokuwa katika mikusanyiko ikiwa ni pamoja na darasani, mistarini au katika vikundi vya majadiliano **isipokuwa Watoto wenye umri chini ya miaka nane (8) na wale wenye matatizo ya mfumo wa hewa kama vile pumu; matatizo ya moyo; Selimundu (Sickle Cell) na wale ambao kwa historia yao ya kiafya walimu wanawafahamu inashauriwa wasivae barakoa.**

- Wanafunzi/Walimu/Watumishi wenye magonjwa ya moyo, selimundu (sickle cell) na wenye magonjwa ya mfumo wa hewa kama vile pumu wapo kwenye hatari zaidi ya kupata madhara ya ugonjwa, hivyo wawe waangalifu zaidi**. Endapo watu hawa watakuwa wanaumwa na kukosa pumzi waepuke mikusanyiko, wavue barakoa kuongeza kiwango cha hewa na watafute msaada wa wataalamu wa Afya.**
- **Uongozi wa shule uhakikishe wanafunzi wote wakati wa kufanya mazoezi ikiwemo kukimbia mchakamchaka hawapaswi kuvaa barakoa**.
- Kwa Shule, Vyuo na Vituo vyenye wanafunzi wenye mahitaji maalumu, walimu wanapaswa kuvaa barakoa maalum zitakazoruhusu mwanafunzi mwenye matatizo ya usikivu kuwasiliana na mwalimu. Aidha, Uongozi kuhakikisha nyenzo za kujimudi (Kiti cha magurudumu, basikeli yenye matairi matatu) vinatakaswa mara kwa mara.
- Wataalam wa Afya wa Mkoa na Halmashauri husika washirikiane na Uongozi wa Shule/Chuo juu ya matumizi sahihi ya barakoa, hatua sahihi za unawaji mikono kwa maji tiririka na sabuni na utumiaji sahihi wa vitakasa mikono kwa wanafunzi, walimu na wafanyakazi wa Shule/Chuo husika.
- Pale ambapo Shule, Vyuo na Vituo vya Elimu vina watumishi wenye taaluma ya afya, inashauriwa watumishi hawa watumike ipasavyo kutoa elimu ya COVID-19 na kusimamia Utekelezaji wa Mwongozo huu kwa kushirikiana na Watalaam wa afya wa Mkoa na Halmashauri zao.
- Ziara za mafunzo nje ya Shule, Vyuo na Vituo vya Elimu zifanyike kwa kuzingatia tahadhari zote za kujikinga na maambukizi ya COVID-19.
- Sherehe zote na makongamano yatakayofanyika ndani na nje ya shule/Vituo vya Elimu (graduation n.k) Uongozi wa shule uzingatie tahadhari zote za kujikinga na kuthibiti maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona
- Wataalamu wa Afya wa Mikoa na Halmashauri zote nchini wanatakiwa wafanye ukaguzi wa mara kwa mara katika shule zilizoko katika maeneo yao ili kuhakikisha tahadhari zote za kujikinga na

maambukizi ya COVID-19 zinazingatiwa kabla ya kufunguliwa Shule na wakati wa masomo ikiwemo kutoa taarifa kwenye mamlaka husika.

Mwongozo huu utaboreshwa mara kwa mara ili kukidhi mahitaji ya wakati husika

Ummy A. Mwalimu (Mb)

**Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto**

**25 Juni, 2020**